East African Scholars Journal of Education, Humanities and Literature
*Abbreviated Key Title: East African Scholars J Edu Humanit Lit*
ISSN: 2617-443X (Print) & ISSN: 2617-7250 (Online)
Published By East African Scholars Publisher, Kenya

OPEN ACCESS

Volume-8 | Issue-6 | Jun- 2025 | DOI: https://doi.org/10.36349/easjehl.2025.v08i06.012

**Review Article**

# Changamoto za Upimaji Jumuishi katika Ufundishaji wa Kiswahili kama Lugha ya Kigeni

Zitaamanzia Said Kididi[1*], Michael Amri Mashauri[2]

[1](Mwanafunzi wa Shahada ya Uzamivu) Idara ya Lugha ya Kiswahili na Isimu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
[2]Idara ya lugha ya Kiswahili na Isimu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

**Article History**
**Received:** 08.05.2025
**Accepted:** 13.06.2025
**Published**: 27.06.2025

**Journal homepage:**
https://www.easpublisher.com

**Quick Response Code**

**Abstract:** Upimaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni umekuwa ukifanyika kwa namna tofautitofauti. Mathalani, upimaji unaojumuisha stadi zote za lugha na upimaji unaozingatia baadhi ya stadi za lugha na kuziacha nyingine. Nadharia Jumuishi ya Lugha inasisitiza upimaji unaojumuisha stadi zote za lugha ili kupata picha halisi ya mafanikio ya mjifunzaji. Licha ya kuwapo kwa tafiti mbalimbali zinazoangazia upimaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni, tafiti hizo hazioneshi changamoto zinazoukabili mchakato wa upimaji kiasi cha kutofautiana kwa kuzingatia au kutozingatia maelezo ya kinadharia. Makala hii imechunguza changamoto za upimaji jumuishi wa stadi za lugha katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni nchini Tanzania. Data za makala hii zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa nyaraka na usaili. Jumla ya walimu kumi na wawili (12) wanaofundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni kutoka katika vituo vitatu (3) walihusika katika utafiti huu. Data zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa data kimaudhui ikiongozwa na Nadharia ya Usababishi iliyoasisiwa na Hume (1739) na kuboreshwa (1748). Matokeo ya utafiti yalibaini changamoto mbalimbali zinazokabili upimaji jumuishi wa stadi za lugha. Changamoto hizo ni: kutofautiana kwa malengo ya wajifunzaji wa lugha, kutofautiana kwa miongozo ya ufundishaji, kukosekana kwa mwongozo rasmi wa Upimaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni, mkazo wa stadi za lugha katika ufundishaji na upimaji, ugumu wa upimaji jumuishi wa stadi zote za lugha na matumizi ya uzoefu binafsi. Kutokana na matokeo hayo, utafiti huu unajenga hoja kuwa kuna haja ya kuweka mikakati ili kuboresha zaidi upimaji jumuishi katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni.

**Keywords:** Lugha Ya Kigeni, Stadi Za Lugha, Upimaji Wa Lugha, Upimaji Jumuishi.

**Copyright © 2025 The Author(s):** This is an open-access article distributed under the terms of the Creative Commons Attribution **4.0 International License (CC BY-NC 4.0)** which permits unrestricted use, distribution, and reproduction in any medium for non-commercial use provided the original author and source are credited.

## 1.0 Utangulizi

Kiswahili kama lugha nyinginezo duniani kimekuwa kikipiga hatua na mahitaji yake kuongezeka kila uchao. Kuongezeka kwa mahitaji na matumizi ya Kiswahili ndani na nje ya Tanzania kumechochea mahitaji makubwa ya kujifunza lugha hii. Mchakato wa ujifunzaji umekuwa ukihusisha ujifunzaji wa stadi zote za lugha ambazo ni kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Mchakato huo hukamilika kwa kuwapima wajifunzaji ili kubaini ikiwa wamefanikiwa kufikia malengo ya kumudu stadi za lugha wanayojifunza. Hivyo, ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni unakwenda sambamba na upimaji ambao hufanyika ili kufahamu mafanikio ya ujuzi wa lugha waliyofikia wajifunzaji. Davies (1990) anafafanua kuwa upimaji lugha hutazama malengo ya ufundishaji kwa mfundishaji na mjifunzaji na kuyaongoza katika kufikia mafanikio. Maelezo hayo yanasisitiza umuhimu wa upimaji wa lugha kwa sababu bila upimaji mfundishaji na mjifunzaji hawawezi kubaini mafanikio waliyofikia. Kwa hiyo, upimaji wa lugha unategemea namna ya ufundishaji wa lugha. Jambo hili linaelezwa na baadhi ya wataalamu kama vile Mao (2022) kuwa upimaji wa lugha hauwezi kutenganishwa na ufundishaji na ujifunzaji wa lugha. Hivyo, katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni, walimu huwapima wajifunzaji ili kubaini kama wamemudu stadi za lugha. Upimaji huu hufanyika kulingana na viwango vya wajifunzaji ili kubaini kama malengo ya ujifunzaji yamefikiwa.

## 2.0 Muhtasari wa Mapitio ya Maandiko kuhusu Upimaji wa Lugha

Ili mjifunzaji wa lugha ya kigeni aweze kutumia lugha katika muktadha halisi wa mawasiliano, hana budi

***Corresponding Author:** Zitaamanzia Said Kididi
(Mwanafunzi wa Shahada ya Uzamivu) Idara ya Lugha ya Kiswahili na Isimu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

kuwa na uelewa wa stadi zote za lugha. Kutokana na uhitaji huo, watafiti wanasisitiza ufundishaji na upimaji jumuishi wa stadi za lugha kwa sababu katika muktadha halisi wa mawasiliano stadi zote hutumika kwa kukamilishana au kutegemeana (Gautam, 2019; Akmal na wenzake, 2020; Khosiyono, 2021).

Ufundishaji na upimaji jumuishi wa lugha ni ule unaohusisha stadi zote za lugha ambazo ni kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Tafiti nyingi za wataalamu kama Oller (1979; Bachman (1990), Lynch (1996), Douglas (2000, 2010), Shohamy (2001) na Sevy-Biloon (2018) zinaonesha umuhimu wa ufundishaji na upimaji jumuishi wa stadi za lugha ili kuleta ufanisi katika ujifunzaji na matokeo yake. Mathalani, Shohamy (2001) na Sevy-Biloon (2018) wanasisitiza kuwa mjifunzaji lugha anapokuwa katika muktadha halisi wa mawasiliano, hutumia stadi zote za lugha ili kuonesha kuwa amefikia umahiri wa kimawasiliano. Hivyo, ujumuishaji wa stadi zote za lugha katika ufundishaji na upimaji wa lugha ya kigeni, inaaminika kuwa ndiyo mbinu bora ya kumwezesha mjifunzaji kumudu matumizi ya lugha katika muktadha halisi.

Katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni ni muhimu kupima uwezo wa wajifunzaji kutumia lugha wanayojifunza. Upimaji huo unapaswa kuwa jumuishi, yaani unaozingatia stadi zote za lugha ambazo ni kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika kwa sababu umilisi wa kila stadi una mchango katika kujenga umilisi wa kimawasiliano. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, ingawa stadi za lugha zinategemeana, matokeo yanayotokana na upimaji wa stadi moja hayawezi kuukilia umilisi wa stadi nyingine kwa usahihi. Hivyo, upimaji wa lugha unaojumuisha stadi zote za lugha ni bora kuliko upimaji unaozitenganisha stadi hizo kwa sababu unamjengea mjifunzaji uwezo wa kutumia stadi zote za lugha kama zinavyotumika katika muktadha halisi wa mawasiliano.

Licha ya tafiti mbalimbali kuonesha umuhimu wa upimaji jumuishi wa stadi za lugha, zipo tafiti kama Rubanza (2010), Hamad (2020), Mgasho (2020) na Ali (2021) zinazoonesha kuwa upimaji jumuishi wa stadi za lugha hauzingatiwi katika baadhi ya miktadha ya ufundishaji Kiswahili kama lugha ya kigeni.

Mathalani, Rubanza (2010) alichunguza masuala ya msingi katika utayarishaji wa majaribio kwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Katika utafiti wake, anadokeza mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa utayarishaji wa majaribio. Mambo hayo ni uaminikaji, uthibitikaji, uhalisia, uhusianifu, matokeo na utekelezaji. Vilevile, anasisitiza kuwa kupima utendaji wa matumizi ya lugha katika muktadha halisi ndicho kigezo kikuu cha majaribio bora ya wajifunzaji wa lugha. Aidha, matokeo ya utafiti wa Rubanza (2010) yanasisitiza kuzingatia lengo kuu la kujifunza lugha wakati wa upimaji ambalo ni mawasiliano. Matokeo yanabainisha kuwa katika muktadha halisi wa mawasiliano, stadi za lugha hazitumiki pwekepweke. Stadi za kusikiliza, kuzungumza, kusoma pamoja na kuandika hutumika kwa kutegemeana na kukamilishana. Msisitizo mkubwa hapa ni kuwa na majaribio yanayojikita katika kupima maarifa ya lugha na matumizi ya lugha katika uhalisia wake. Hii ni kwa sababu, kumpima mjifunzaji katika stadi pwekepweke kunaweza kumsababishia changamoto wakati wa kuwasiliana katika muktadha halisi.

Hamadi (2020) alifanya utafiti kutathmini uthabiti wa mitihani ya Kiswahili kwa wageni. Matokeo ya utafiti wake yalibainisha kuwa, mitihani ilikidhi kigezo cha uthabiti wa kimaudhui kwani kwa kiwango kikubwa maudhui ya mitihani yaliendana na maudhui yaliyomo katika vitabu vya kufundishia. Hata hivyo, pamoja na mitihani hiyo kubainika kuwa inaendana na maudhui yaliyomo katika vitabu vya kufundishia Kiswahili kama lugha ya kigeni, mitihani hiyo haikupima stadi ya kusikiliza na kuzungumza. Licha ya msisitizo wa wataalamu kuwa stadi hizo ni muhimu katika mawasiliano, waandaaji wa mitihani walijikita katika kupima sarufi, msamiati, stadi ya kusoma pamoja na kuandika.

Mgasho (2020) aliangazia mkabala unaotumika katika utungaji wa mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni. Matokeo ya utafiti wake yalibainisha kuwa kuna mikabala ya aina mbili. Mkabala wa kwanza ni ule unaopima stadi moja na mkabala wa pili unaopima stadi mchanganyiko kwa wakati mmoja. Pia, matokeo yanaonesha kuwa walimu walikuwa na uelewa kuhusu mikabala ya upimaji wa lugha za kigeni. Vilevile, ilibainika kuwa mkabala unaopima stadi mchanganyiko za lugha kwa wakati mmoja ndio uliokuwa unatumika zaidi katika uandaaji wa mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni. Hii ilitokana na mtazamo wa walimu kuwa mkabala huo unafaa katika kutoa matokeo chanya ya wajifunzaji.

Naye Ali (2021) alitathmini msingi wa uhalisia katika mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni. Katika matokeo ya utafiti wake anabainisha kuwa walimu walikuwa na uelewa wa wastani kuhusu msingi wa uhalisia katika uandaaji wa mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni. Pia, matokeo yalibainisha kuwa, licha ya uelewa wa wastani walionao walimu kuhusu msingi wa uhalisia katika utungaji wa mitihani, msingi huo haukuzingatiwa katika uandaaji wa mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni. Hali hii ilitokana na wajifunzaji kutoandaliwa kwa kutumia stadi zote za lugha ambazo ni kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Jambo hili limebainika kujitokeza katika ufundishaji na upimaji. Vilevile, mkabala wa mawasiliano umebainika kutozingatiwa ikiwa ni pamoja na mbinu za ufundishaji na upimaji kutojikita katika kumjengea mjifunzaji uwezo wa kuwasiliana katika muktadha halisi. Aidha, walimu walibainika kutumia

zaidi uzoefu wao katika uandaaji wa mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni.

Kahindi (2022) alichunguza ikiwa kuna uwiano kati ya malengo mahususi na mazoezi ya stadi ya kuzungumza katika darasa la Kiswahili kama lugha ya kigeni. Matokeo ya utafiti wake yalionesha kuwa, kwa kiasi kikubwa walimu wanaongozwa na malengo mahususi yaliyomo katika kitabu cha kufundishia katika ufundishaji wao. Pia, utafiti ulibaini kuwa 61% ya mazoezi yaliyotolewa na walimu yaliwiana na malengo mahususi yaliyomo kwenye kitabu cha kufundishia. Vilevile, ilibainika kuwa 13% ya mazoezi yaliyotolewa na walimu hayakuwiana na malengo mahususi yaliyomo kwenye kitabu cha kufundishia. Aidha, 26% ya walimu walibainika kutotoa mazoezi wakati wa ufundishaji wa stadi ya kuzungumza kinyume na malengo ya ufundishaji. Pamoja na hayo, utafiti ulibaini kuwa baadhi ya walimu hawakuzingatia mpangilio wa malengo mahususi wakati wote. Hii ni kwa sababu baadhi ya mada ndogo walizozifundisha hazikuendana na mpangilio wa malengo mahususi yaliyomo kwenye kitabu.

Kwa ujumla, machapisho yaliyopitiwa yanabainisha kuwa bado kuna ukosefu wa ufanisi katika kutekeleza upimaji jumuishi wa stadi za lugha katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni. Hali hii inafanya mchakato mzima wa ufundishaji kutokukamilika kwa jinsi inavyotakiwa kulingana na maelezo ya kinadharia. Kukosekana kwa ukamilifu na ufanisi huo kunaibua shauku ya kutaka kufahamu changamoto za upimaji jumuishi zinazochangia hali iliyopo katika upimaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni. Hivyo, utafiti huu unalenga kuchunguza changamoto zinazojitokeza katika upimaji jumuishi wa stadi za lugha katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni.

## 3.0 Nadharia

Uchanganuzi wa data za makala hii umeongozwa Nadharia ya Usababishi. Nadharia hii iliasisiwa na Hume mwaka 1739 na kuboreshwa mwaka 1748 akiwa na mtazamo kuwa chanzo na athari hutokana na uzoefu wa kimaisha. Anaeleza kuwa maarifa yetu yote yanatoka katika uzoefu wetu wa maisha, na uhusiano ndio unaochangia kutokea kwa jambo. Mawazo ya Hume yanaonesha kuwa usababishi unatokana na mazoea ya kitabia kuliko muunganiko wa matukio. Mtazamo huu unafanya usababishi kuwa tukio la kisaikolojia zaidi kuliko uhalisia. Nadharia hii iliendelezwa na wataalamu mbalimbali. Miongoni mwao ni Pearl (2000) aliyeiboresha kwa kusisitiza upimaji wa kisayansi wa mahusiano ya kiusababishi. Alitumia mifumo ya kitakwimu na grafu katika kueleza namna sababu zinavyoweza kuathiri matokeo. Anaeleza kuwa kuna uhusiano tegemezi wa matukio na wajibu wa watafiti ni kufafanua visababishi vya matukio. Naye Goodman na wenzake (2011) waliiendeleza Nadharia ya Usababishi kwa kuiboresha wakieleza kuwa imejikita katika uhusiano wa matukio. Wanaeleza kuwa ulimwengu umeundwa na mkusanyiko wa mifumo sababishi, na katika kila mfumo sababishi kuna fahiwa sababishi zinazoonekana. Aidha, Woodward (2021) anaiendeleza Nadharia ya Usababishi kwa kusisitiza kuwa usababishi unatakiwa kutazamwa na kueleweka kwa kuchunguza matokeo. Anafafanua kuwa kuelewa usababishi kunahitaji kuchunguza namna mabadiliko ya kisababishi yanavyoathiri matokeo katika mfumo wa kimwingiliano. Hivyo, wataalamu walioiendeleza Nadharia ya Usababishi wamejikita katika hoja kuu kwamba matukio hutokea kwa kutegemeana tofauti na mtazamo wa mwasisi kwamba usababishi ni tukio la kisaikolojia. Nadharia hii ina misingi miwili ambapo wa kwanza unafafanua kuwa kisababishi lazima wakati wote kilete athari na wa pili unaeleza kuwa jukumu la mwisho la mtafiti ni kufafanua uwezekano wa kuzuia kisababishi iwapo gharama za athari ni kubwa. Licha ya Nadharia ya Usababishi kuwa na misingi miwili, msingi wa kwanza pekee ndio uliotumika katika utafiti huu ili kufikia lengo kuu la makala hii ambalo ni kufafanua changamoto zinazoukabili upimaji jumuishi wa stadi za lugha katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni.

## 04. Methodolojia

Utafiti huu ulifanyika nchini Tanzania katika vituo vitatu vinavyofundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni ambavyo katika makala hii vinabainishwa kama vituo X, Y na Z. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa nyaraka na mbinu ya usaili. Mbinu ya uchambuzi wa nyaraka ilihusisha mitihani minne kutoka katika kila kituo ambapo ilipatikana jumla ya mitihani kumi na miwili (12) ya miaka 2013, 2015, 2017 na 2019. Mbinu ya usaili ilitumika kupata data kutoka kwa watoataarifa kumi na wawili (12) ambao ni walimu wanaofundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni kutoka katika vituo husika. Kila kituo kiliwakilishwa na walimu wanne (04) ambao pia huandaa mitihani kwa ajili ya kuwapima wajifunzaji. Walimu hao walipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji nasibu. Mbinu ya usaili ilitekelezwa kwa kutumia aina ya usaili nusufunge ambapo mtafiti alitumia mwongozo wa maswali kuwauliza walimu kuhusu changamoto zinazokabili mchakato wa upimaji wa stadi za lugha katika muktadha husika nao walizibainisha. Aidha, data za utafiti huu zimechambuliwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa data kimaudhui ikiongozwa na Nadharia ya Usababishi.

## 5.0 Changamoto za Upimaji Jumuishi wa Stadi za Lugha katika Ufundishaji wa Kiswahili kama Lugha ya Kigeni

Matokeo ya utafiti huu yamebainisha kuwa upimaji wa stadi za lugha katika mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni unatofautiana baina ya vituo hivi. Tofauti hizo zinaoneshwa katika Jedwali Na.1.

**Jedwali Na. 1: Tofauti za Upimaji wa Stadi za Lugha**

| Mwaka | Vituo | Stadi za Lugha | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kusikiliza | Kuzungumza | Kusoma | Kuandika |
| 2013 | X | | | √ | √ |
| | Y | | | √ | √ |
| | Z | √ | √ | √ | √ |
| 2015 | X | | | √ | √ |
| | Y | | | √ | √ |
| | Z | √ | √ | √ | √ |
| 2017 | X | | | √ | √ |
| | Y | √ | √ | √ | √ |
| | Z | √ | √ | √ | √ |
| 2019 | X | | | √ | √ |
| | Y | √ | √ | √ | √ |
| | Z | √ | √ | √ | √ |

Kutokana na data katika Jedwali Na. 1, imebainika kuwa stadi za kusoma na kuandika zimepimwa katika vituo vyote kwa miaka yote minne. Pia, stadi za kusikiliza na kuzungumza zimepimwa kwa miaka yote katika kituo Z, miaka miwili katika kituo Y wakati katika kituo X hazikupimwa kabisa. Kutokana na data hiyo, tofauti na upimaji wa stadi za lugha katika kituo X na Y unaoonekana kutozingatia Nadharia Jumuishi ya Lugha, upimaji wa stadi za lugha katika kituo Z pekee ndio unaoonekana kuendana na Nadharia Jumuishi ya lugha. Hii ni kwa sababu vituo X na Y vimebainika kupima zaidi stadi za kusoma na kuandika huku vikiacha stadi ya kusikiliza na kuzungumza au kuzipima kwa kiwango kidogo kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 1. Aidha, kituo Z kimebainika kupima stadi zote za lugha ambazo ni kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika wakati wote. Upimaji katika kituo Z unaunga mkono mawazo ya Powers na Powers (2014) na Asafo-Adjei (2022) wanaosisitiza upimaji wa stadi zote za lugha kwa sababu stadi hizo hukamilishana katika muktadha halisi wa matumizi ya lugha. Data katika Jedwali Na. 1 zinadhihirisha kuwa upimaji wa stadi za lugha unatofautiana baina ya vituo vinavyofundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni. Hali hii imesababishwa na changamoto mbalimbali zinazokabili mazingira ya ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni nchini Tanzania. Changamoto hizo zinafafanuliwa katika vipengele vinavyofuata.

**5.1 Kutofautiana kwa Miongozo ya Ufundishaji**

Utafiti huu ulibaini kuwapo kwa tofauti katika miongozo ya kufundishia. Kwa kuwa upimaji hutegemea ufundishaji, watoataarifa walifafanua kuwa huwapima wajifunzaji kutokana na namna wanavyowafundisha. Hali hii inasababisha upimaji wa stadi za lugha katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni kutofautiana kati ya vituo husika kwa sababu kila kituo kina mwongozo wake wa kufundishia. Katika kulifafanua hili, baadhi ya watoataarifa walieleza kama ifuatavyo:

Mtoataarifa wa kwanza:

Sisi tuna miongozo ambayo tunaiandaa kulingana na mahitaji ya kozi. Pia huwa tunaandaa miongozo mara kwa mara kwa sababu malengo na mahitaji ya wajifunzaji hutofautiana. Kwa hiyo upimaji pia hutegemea mwongozo unaotumika kwa wakati husika.
**Chanzo**: Uwandani (2022)

Mtoataarifa wa pili:

Hakuna mfumo wala mwongozo wa nchi unaotulazimisha kufanya jambo kwa namna fulani isipokuwa uelewa wa taaluma hii kidunia. Kama taasisi au walimu wanapambana kuendana na mifumo ya kidunia ya ufundishaji na upimaji pia.
**Chanzo**: Uwandani (2022)

Maelezo ya watoataarifa yanadhihirisha kuwa kutofautiana kwa upimaji wa stadi za lugha kwa wajifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni kunachangiwa kwa kiasi kikubwa na kutofautiana kwa miongozo ya kufundishia. Maelezo hayo yanaonesha uhitaji wa vituo vyote vinavyofundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni kutumia mwongozo mmoja wa ufundishaji ili kufanya upimaji kuwa wa aina moja au kutotofautiana sana baina ya vituo hivyo.

Changamoto ya kutofautiana kwa miongozo inaweza pia kuleta athari mbalimbali katika upimaji wa stadi za lugha. Miongoni mwa athari hizo ni kukosekana kwa vigezo maalumu vya kutathmini ujuzi wa lugha vinavyoweza kutumika katika vituo vyote. Hii ni kwa sababu kila kituo kina vigezo vyake kulingana na mwongozo unaotumika.

Lantolf na Poehner (2004) wanaeleza kuwa bila mfumo wa kufundishia ulio bora, walimu wanaweza

kufanya tathmini za wajifunzaji kwa kutumia vigezo tofauti; na hivyo, kusababisha tofauti katika utoaji wa alama na maoni. Tofauti hii inaweza kuwafanya wajifunzaji wapate taarifa zisizo sahihi kuhusu ufanisi wao katika lugha wanayojifunza, kwani maamuzi kuhusu uelewa wao wa lugha yanaweza kutofautiana kutoka kwa mwalimu mmoja au taasisi moja hadi nyingine.

Vilevile, kutofautiana kwa miongozo ya kufundishia kunaweza kuzuia ujumuishaji wa ujuzi wa stadi kuu nne za lugha, yaani kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika kwa sababu vituo vinaweza kuwa na mtazamo tofauti pia kuhusu uzito wa kila stadi. Programu bora ya lugha inahitaji ujumuishaji wa ujuzi wa stadi zote za lugha wenye usawa (Richards na Rodgers, 2001). Hata hivyo, bila mwongozo ulioandaliwa vizuri, kuna hatari ya kupuuza mojawapo ya stadi hizi za lugha na hivyo kusababisha umilisi wa lugha usio na usawa.

Kutokana na ukweli kuwa upimaji huathiriwa na mchakato wa ufundishaji, kutofautiana kwa miongozo ya ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni kati ya vituo husika ni changamoto inayoukabili ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni. Ili kuepuka changamoto hii, ni vyema vituo vyote kutumia mwongozo rasmi ili kuimarisha mchakato mzima wa ujifunzaji lugha ikiwa ni pamoja na upimaji.

**5.2 Kutofautiana kwa Malengo ya Wajifunzaji wa Lugha**

Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa upimaji wa stadi za lugha katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni unakabiliwa na changamoto ya kutofautiana kwa malengo ya wajifunzaji wa lugha. Hii ni kwa sababu malengo ya wajifunzaji ndiyo huongoza mchakato wa ufundishaji. Tofauti hizo zinadhihirishwa na maelezo yaliyotolewa na watoataarifa 04 kati ya 12 ambao ni walimu waliohusika katika utafiti huu. Watoataarifa hao ni wale waliobainika kupima stadi zote za lugha, yaani kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Wakitilia mkazo upimaji wa stadi zote za lugha hasa kusikiliza na kuzungumza, baadhi yao walieleza:

Mtoataarifa wa kwanza:

> Malengo ya wajifunzaji wengi wa lugha ni kuwasiliana kwa kutumia lugha wanayojifunza. Kwa kuwa njia kuu ya mawasiliano ni mazungumzo, wajifunzaji wengi hujifunza lugha ili waweze kuwasiliana kwa kutumia njia hiyo. Kwa hiyo tunapima stadi ya kusikiliza na kuzungumza kwa sababu ndiyo msingi wa mawasilaiano. Ili mjifunzaji aweze kuzungumza na mtu mwingine ni lazima amsikilize na kumwelewa ndipo naye amjibu au aendeleze mazungumzo.
> **Chanzo**: Uwandani (2022)

Mtoataarifa wa pili:

> Ni muhimu kupima stadi zote lakini zaidi kusikiliza na kuzungumza kwa sababu wajifunzaji wanahitaji kuishi na jami ya Waswahilii. Kwa mfano mapadre na wachungaji wanajifunza lugha ya Kiswahili ili waweze kuwahubiria waumini na mara nyingi mahubiri hufanyika kwa njia ya kuzungumza. Hivyo, ni vema kumpima ili kubaini namna wajifunzaji wanavyoweza kutamka, kuzungumza na kuelewa Kiswahili.
> **Chanzo**: Uwandani (2022)

Data hiyo inadhihirisha kuwa walimu wanaamini kuwa kusikiliza na kuzungumza ni njia kuu ya mawasiliano. Hii ni kwa sababu, pamoja na kudai kuwa ni muhimu kupima stadi zote, msisitizo wao upo katika stadi ya kusikiliza na kuzungumza. Licha ya maelezo yaliyotolewa na watoataarifa hao, watoataarifa wengine ambao walijikita katika upimaji wa stadi za kusoma na kuandika walieleza sababu zinazochangia upimaji wa aina hiyo. Miongoni mwao walibainisha:

Mtoataarifa wa kwanza:

> Lengo kuu la mjifunzaji lugha ni kuwasiliana kwa njia ya mazungumzo, lakini ni muhimu pia kupima stadi ya kuandika kwa sababu kuandika ni hatua ya juu baada ya hatua za awali za kusikiliza, kuzungumza na kusoma kukamilika.
> **Chanzo**: Uwandani (2022)

Mtoataarifa wa pili:

> Wajifunzaji wengine wana malengo ya kuwa watafiti na waandishi wa kazi za Kiswahili. Hawa lazima wapimwe ili kujiridhisha juu ya kuimarika kwao katika usomaji na uandishi wa kazi mbalimbali.
> **Chanzo**: Uwandani (2022)

Kwa kuzingatia data hii, ni wazi kwamba malengo tofauti ya wajifunzaji wa lugha za kigeni yanaathiri kwa kiasi kikubwa upimaji wa ujuzi wao wa lugha. Kama maelezo ya msingi wa kwanza wa Nadharia ya Usababishi yanavyofafanua kuwa kisababishi lazima kilete athari wakati wote, ndivyo hali halisi ya upimaji wa stadi za lugha katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni inavyodhihirika. Hii ni kutokana na mchakato wa upimaji wa stadi za lugha kufanyika kwa kuzingatia malengo mbalimbali ya wajifunzaji kama vile kuwasiliana, kufanya tafiti mbalimbali kuhusu lugha ya

Kiswahili pamoja na kuandika kazi zinazohusu lugha hiyo.

Maelezo kuhusu upimaji kuathiriwa na malengo ya wajifunzaji wa lugha yanaunga mkono maelezo ya Gardner (1985) na Dornyei (2001) yanayofafanua umuhimu wa kuzingatia malengo ya wajifunzaji katika upimaji kwani huwapa motisha. Wameeleza kwamba, ikiwa wanafunzi wanaona uhusiano wa moja kwa moja kati ya upimaji na malengo yao binafsi, kuna uwezekano mkubwa wa kuwa na motisha ya ndani, hivyo, kuleta matokeo bora.

Kwa ujumla, malengo ya wajifunzaji wa lugha za kigeni yanaathiri kwa kiasi kikubwa namna ya upimaji wa ujuzi wao wa lugha. Uzingatiaji wa malengo ya wajifunzaji katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni, umechangia kwa kiasi kikubwa upimaji wa stadi za lugha kutofautiana baina ya vituo husika.

**5.3 Kukosekana kwa Mwongozo Rasmi wa Upimaji wa Kiswahili kama Lugha ya Kigeni**

Matokeo ya utafiti huu pia yamebaini kuwa kukosekana kwa mwongozo wa upimaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni, ni miongoni mwa changamoto zinazoukabili upimaji jumuishi wa stadi za lugha katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni. Jambo hilo linasababisha vituo vinavyofundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni kutofautiana hasa katika ujumuishaji wa stadi za lugha katika upimaji. Tofauti hizo zinasababisha kila kituo kubuni vigezo vyake na namna ya kuendesha shughuli za upimaji kwa jinsi ambavyo wanaona inafaa. Katika kulifafanua hili baadhi ya watoataarifa walieleza:

Mtoataarifa wa kwanza:

> Hakuna mwongozo unaolekeza namna ya kupima. Hivyo, upimaji hufanyika kutokana na mada zilizofundishwa darasani.
> **Chanzo**: Uwandani (2022)

Mtoataarifa wa pili:

> Katika kituo chetu hakuna mwongozo rasmi wa upimaji. pia hatujawahi kupokea maelekezo yoyote kuhusu namna ya kuwapima wajifunzaji. Hivyo huwa ninatumia kitabu cha kufundishia.
> **Chanzo**: Uwandani (2022)

Kutokana na data hii, ni wazi kwamba mada zinazofundishwa ndizo huwaongoza wafundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni katika upimaji wa stadi za lugha hiyo. Upimaji huo unaonekana kutokuwa na muundo rasmi kwani kila kituo kina namna yake ya kupima kutokana na mada zilizofundishwa ambazo hutegemea malengo na mahitaji ya wajifunzaji. Pia, kukosekana kwa mwongozo wa kitaifa wa namna ya upimaji kunawafanya walimu kubuni mbinu zao binafsi za upimaji ili kujaribu kuendana na mabadiliko ya kiulimwengu. Kama maelezo ya Nadharia ya Usababishi yanavyofafanuliwa katika msingi wa kwanza kuwa kisababishi wakati wote huleta athari, ndivyo namna ya upimaji wa stadi za lugha katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni inavyoathiriwa na kutokuwa na na mwongozo rasmi wa upimaji. Katika muktadha wa ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni hali hii imesababisha mitihani ya upimaji wa stadi za lugha kutofautiana kwa sababu kila mwalimu anapima kutokana na uelewa alionao kuhusu upimaji wa stadi hizo.

Kuwa na mwongozo unaoelekeza namna ya upimaji wa stadi za lugha katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni ni muhimu. Hii ni kwa sababu utawasaidia wafundishaji kupanga mbinu na vigezo vya kutumia katika upimaji wa stadi za lugha. Brown (2004) anaeleza kuwa vigezo vya upimaji vilivyowekwa vizuri huwasaidia walimu kufanya maamuzi sahihi kuhusu viwango vya ufasaha wa wajifunzaji na kutengeneza mikakati inayofaa ya mafunzo. Hivyo, kukosekana kwa mwongozo sahihi wa upimaji kunaweza kuathiri mchakato mzima wa upimaji na matokeo ya ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni.

**5.4 Kukosekana kwa Msisitizo wa baadhi ya Stadi za Lugha katika Ufundishaji na Upimaji**

Upimaji wa stadi zote za lugha ni muhimu katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni kwani husaidia kupata picha halisi ya mafanikio ya wajifunzaji. Matokeo ya utafiti huu yamebainisha kuwa upimaji wa stadi za lugha katika muktadha wa ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni unakabiliwa na changamoto ya kukosekana kwa msisitizo wa baadhi ya stadi za lugha. Mmoja kati ya watoataarifa alieleza yafuatayo:

> Kwakuwa wajifunzaji wapo katika mazingira halisi ya ujifunzaji, wanapata fursa ya kuchangamana na wazawa na na kufanya nao mawasiliano kwa kusikiliza na kuzungumza nje ya darasa. Hivyo, msisitizo zaidi tunaweka katika stadi ya kusoma na kuandika.
> **Chanzo**: Uwandani (2022)

Data hiyo inadhihirisha kuwa stadi za kusikiliza na kuzungumza hazizingatiwi katika upimaji wa stadi za lugha katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni. Hali hii inatia shaka ya kwamba huenda stadi hizo

hazizingatiwi pia katika ufundishaji kwa sababu wafundishaji wanaamini kuwa, katika muda wote wa ujifunzaji stadi hizo zinatumika na hivyo ni rahisi kwa wajifunzaji kuzipata vizuri wawapo nje ya darasa. Kama Nadharia ya Usababishi inavyofafanua, ni wazi kuwa kutopimwa kwa baadhi ya stadi za lugha katika mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni kunasababishwa na changamoto ya mkazo kuwekwa katika baadhi ya stadi za lugha.

Bila kuwapima wajifunzaji wa lugha katika stadi zote za lugha, ni vigumu kujua kama wajifunzaji hao wamefanikiwa kumudu stadi zote za lugha wawapo nje ya darasa. Hivyo, katika muktadha wa ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni ni muhimu kufundisha na kupima stadi zote za lugha ili kujua kama malengo yamefikiwa.

Katika mazingira ya ufundishaji wa lugha, stadi zote za lugha, yaani kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika zinapaswa kutiliwa mkazo sawa kwani kila moja ina umuhimu katika kukamilisha mawasiliano. Kukosekana kwa mkazo sawa kwa stadi zote za lugha kunaweza kuathiri upimaji wa ujuzi wa lugha wa wajifunzaji. Ellis (1994) anaeleza kuwa kujifunza lugha ni mchakato wenye pande nyingi, hivyo, kupuuza upande wowote kunaweza kupunguza uelewa wa mjifunzaji wa lugha husika. Kutoipa kipaumbele cha kutosha stadi fulani ya lugha katika ufundishaji, kunaathiri namna stadi hiyo itakavyopimwa wakati wa kufanya tathmini.

Miongoni mwa athari hizo ni wajifunzaji kumudu vizuri stadi fulani za lugha na kukabiliwa na changamoto katika stadi nyingine. Pia, matokeo yanaweza kutoa picha isiyokuwa sahihi ya ujuzi wa lugha wa wajifunzaji. Hii itatokana na maoni na maamuzi kuzingatia stadi ambazo zimefundishwa na kupimwa. Ikiwa walimu wanazingatia hasa stadi ya kusoma na kuandika katika ufundishaji, ni wazi kuwa upimaji utazingatia stadi hizo na kupuuza stadi ya kusikiliza na kuzungumza (Alderson, 2000).

Mbinu za ufundishaji wa lugha za kigeni zinazozingatia ujumuishaji wa stadi zote za lugha zina manufaa si tu katika upimaji wa lugha, bali hata kwa maendeleo ya ujuzi wa kutumia lugha katika mazingira halisi. Hivyo, ni muhimu kufundisha na kupima stadi zote za lugha ili kumjengea mjifunzaji uwezo wa kutumia lugha aliyojifunza.

### 5.5 Ugumu wa Upimaji Pamwe wa Stadi zote za Lugha

Ugumu wa kupima stadi zote za lugha kwa wakati mmoja ni changamoto nyingine inayoukabili upimaji wa stadi za lugha katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni. Hii inatokana na muktadha halisi wa upimaji kubainisha kuwa mitihani hiyo inapima stadi mbili tu na mara chache stadi zote nne kwa wakati mmoja. Katika kufafanua hoja hii baadhi ya watoataarifa waliotoa mfano wa stadi ya kuzungumza walieleza yafuatayo:

Mtoataarifa wa kwanza:

> Kutojumuishwa kwa stadi ya kuzungumza wakati wa upimaji kunasababishwa na muda na mazingira.
> **Chanzo**: Uwandani (2022)

Mtoataarifa wa pili:

> Ni vigumu kujumuisha stadi ya kuzungumza na stadi nyingine kutokana na stadi hiyo kuhitaji muda mrefu wa kuipima tofauti na stadi nyingine.
> **Chanzo**: Uwandani (2022)

Data kutoka kwa watoataarifa inadhihirisha kwamba upimaji wa stadi ya kuzungumza unahitaji mazingira maalumu pamoja na muda wa kutosha. Kutojumuishwa kwa stadi ya kuzungumza katika upimaji wa stadi za lugha katika mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni kunachangiwa na ukosefu wa muda wa kutosha kuwapima wajifunzaji. Mitihani huwa na muda maalumu uliopangwa kufanyika bila kuzingatia kuwa stadi fulani itatumia muda gani. Stadi ya kuzungumza inahitaji muda wa kutosha wakati wa kuipima kwa sababu mfumo wake ni wa majibizano kati ya mjifunzaji na mpimaji. Pia, vituo vinavyotoa huduma ya ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni vimebainika kuwa na mazingira duni ambayo hayaendani na maendeleo ya sayansi na teknolojia na hivyo kutokuwa rafiki katika kupima stadi ya kuzungumza. Nadharia ya Usababishi katika msingi wake wa kwanza inasisitiza kuwa athari yoyote lazima itokane na sababu fulani. Hoja hii inaendana na maelezo hayo kwasababu katika utafiti huu imebainika kuwa, stadi ya kuzungumza haijumuishwi katika upimaji kwa sababu ya ugumu wa upimaji wa stadi hiyo unaochangiwa na kukosa muda wa kutosha pamoja na mazingira duni ya vituo husika.

Hoja hizo zinaunga mkono utafiti wa Semiun na Luruk (2020) uliobainisha kuwa upimaji wa Kiingereza kama lugha ya kigeni kwa wajifunzaji wa darasa la saba nchini Kupang haukujumuisha stadi ya kusikiliza na kuzungumza. Utafiti huo ulibainisha sababu zilizochangia stadi hizo kutopimwa kuwa ni pamoja na masuala ya kiutawala, kutokuwa na muda wa kutosha na gharama za uendeshaji wa mchakato huo. Haya yote yanachangia upimaji lugha kutoendana na kasi ya maendeleo ya sayansi na teknolojia ya kiulimwengu.

### 5.6 Kutegemea Uzoefu Binafsi

Utafiti umebaini kuwa utegemezi katika uzoefu binafsi katika upimaji ni miongoni mwa changamoto zinazoukabili upimaji wa stadi za lugha katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni. Katika muktadha wa ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni stadi ya kusikiliza na kuzungumza zimebainika kupimwa kwa kiwango kidogo kuliko stadi za kusoma na kuandika. Hali hii imebainika kuchangiwa na mtazamo wa wafundishaji kuwa mtihani ni ule wa kusoma na kuandika. Baadhi ya watoataarifa walieleza kuwa;

Mtoataarifa wa kwanza:

| |
|---|
| Mara nyingi stadi ya kuzungumza haipimwi kwa sababu tu ya mazoea. Kwakuwa ufundishaji hufanyika kwa njia ya mazungumzo, wajifunzaji hupata muda wa kutosha kujifunza kuzungumza lugha ya Kiswahili kwa vitendo. Hivyo, hakuna haja ya kupima stadi hiyo kwa sababu wajifunzaji huimudu vizuri kupitia maisha yao ya kila siku.<br>**Chanzo**: Uwandani (2022) |

Mtoataarifa wa pili:

| |
|---|
| Kwa kawaida tumezoea kuwa mtihani ni wa kusoma na kuandika. Kwa uzoefu wangu naona si lazima wajifunzaji kupimwa katika kusikiliza na kuzungumza.<br>**Chanzo**: Uwandani (2022) |

Kwa kuzingatia data hii, ni wazi kuwa katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni wapimaji hutegemea zaidi uzoefu binafsi kukamilisha mchakato wa upimaji. Hii ni changamoto inayosababisha upimaji huo hutofautiana kulingana na uzoefu walionao wapimaji. Katika muktadha huu wapimaji wamebainika kutojumuisha stadi za kusikiliza na kuzungumza kwa kuwa uzoefu wao kuhusu upimaji ni ule wa kusoma na kuandika. Pamoja na kudai kujikita katika upimaji wa aina hiyo, mitihani mingine ilibainika kupima stadi ya kusoma na kuandika kwa kutumia maswali yanayohusu sarufi na msamiati zaidi kuliko maswali ya kusoma kwa ufahamu na kuandika.

Maelezo hayo yanakubaliana na Nadharia ya Usababishi kuwa kila athari lazima itokane na sababu. Hili linadhihirika katika upimaji wa stadi za lugha katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni kwani uzoefu binafsi wa kupima stadi za lugha unaathiri mchakato mzima wa upimaji jumuishi wa stadi za lugha. Kwa mujibu wa watoataarifa, upimaji wa stadi za lugha unatokana na uzoefu walionao wakiamini kuwa wajifunzaji wa lugha wanapomudu kujibu maswali ya sarufi na msamiati, yanayohusisha kusoma na kuandika wanakuwa wamepimwa ujuzi wao wa lugha kikamilifu. Hivyo, stadi za kusikiliza na kuzungumza zinapimwa kwa kiwango kidogo na wakati mwingine hazipimwi kabisa.

Kutegemea zaidi uzoefu binafsi kupima stadi za lugha katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni kunaweza kusababisha athari mbalimbali katika mchakato mzima wa upimaji jumuishi wa stadi za lugha. Miongoni mwa athari hizo ni kuendeleza upimaji wa kimapokeo ambao hauwajengei wajifunzaji uwezo wa kutumia lugha ya Kiswahili katika muktadha halisi wa mawasiliano, badala yake kujua zaidi sarufi ya lugha husika.

Upimaji wa stadi za lugha kutokana na uzoefu binafsi unaweza kudumaza ubunifu katika mbinu za upimaji jumuishi wa stadi za lugha. Ubunifu katika upimaji wa lugha unahusisha matumizi ya zana na mbinu za kisasa. Wapimaji wanapojikita katika uzoefu binafsi ambao mara nyingi huhusisha upimaji wa kimapokeo, wanashindwa kubuni zana na mbinu za upimaji jumuishi zinazoendana na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Katika ulimwengu wa utandawazi, matumizi ya zana na mbinu za kisasa, kwa mfano, vyombo vya habari, mazingira halisi pamoja na mitandao yanachangia kuimarisha ujuzi wa kutumia lugha katika muktadha halisi wa mawasiliano kwa sababu huhusisha zaidi utendaji. Upimaji unaohusisha utendaji ni mbinu bora ya kuwapima wajifunzaji wa lugha kwa sababu unapima uwezo wa wajifunzaji kutumia lugha kwa kuzingatia muktadha halisi wa mawasiliano (Noorozi na Taheri, 2022).

Upimaji ulio bora hauwezi kufanyika ikiwa wapimaji hawana maarifa ya kutosha kuhusu namna ya kupima stadi za lugha. Hili linaonesha wazi kuwa kuna haja ya wafundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni ambao pia hushughulika na upimaji wa lugha kuwa na maarifa kuhusu upimaji jumuishi wa stadi za lugha. Ufanisi wa upimaji wa lugha hutegemea maarifa ya upimaji wa lugha waliyonayo wapimaji. De Silva (2020) anasisitiza kuwa upimaji wa lugha unapaswa kufanyika kwa kuzingatia ujuzi na maarifa yanayohusu upimaji wa lugha. Ukosefu wa maarifa kuhusu upimaji jumuishi wa stadi za lugha kwa walimu wa Kiswahili kama lugha ya kigeni una athari kwa wafundishaji na wajifunzaji. Athari hizo huanzia katika kupanga na kuchagua maudhui, idadi ya maswali, mbinu za upimaji na namna ya kutoa alama kwa wajifunzaji.

## 6.0 Hitimisho

Makala hii imechunguza changamoto za upimaji jumuishi wa stadi za lugha katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni. Matokeo ya data zilizokusanywa yanaonesha kwamba stadi za lugha zinapimwa kwa kutofautiana kati ya vituo vinavyohusika. Imebainika kuwa stadi zinazopimwa zaidi ni za kusoma na kuandika kuliko stadi za kusikiliza na kuzungumza. Hali hii imechangiwa na changamoto

mbalimbali kama ilivyobainishwa katika makala hii. Licha ya changamoto hizo, upimaji jumuishi wa stadi za lugha katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni ni muhimu. Hii ni kwa sababu lugha inapotumika katika muktadha halisi, hutumika kama kitu kizima na si kwa kutenganisha stadi zake. Kutowapima wajifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni katika stadi zote za lugha kutawafanya washindwe kumudu kuitumia lugha hiyo katika muktadha halisi wa mawasiliano. Ili kukabiliana na changamoto hizo, inapendekezwa kwamba vyombo vyenye mamlaka likiwamo Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), vishirikiane na wataalamu wa upimaji wa lugha na wafundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni kutoka katika vituo mbalimbali kuhakikisha kuwa wanaandaa mwongozo rasmi wa ufundishaji na upimaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni. Mwongozo huo unapaswa kuhakikisha kuwa stadi zote za lugha zinajumuishwa katika ufundishaji na upimaji kama Nadharia Jumuishi ya Lugha inavyoelekeza. Suala hili liende sambamba na usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa matumizi ya mwongozo huo katika vituo vinayohusika na ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni nchini Tanzania. Pia, vyombo hivyo vinapaswa kuhakikisha kuwa walimu wanaofundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni wanapata mafunzo kuhusu maarifa ya upimaji jumuishi wa stadi za lugha na umuhimu wake kumwezesha mjifunzaji kumudu lugha anayojifunza. Aidha, kwa kuwa suala la uboreshaji wa miundombinu ili kuendana na maendeleo ya sayansi na teknolojia si la ghafla, ni vema vituo husika vizingatie upimaji jumuishi wa stadi za lugha kwa kutumia mbinu zinazofaa kulingana na mazingira. Kwa kufanya haya, ufundishaji na upimaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni utakuwa wenye tija na utawasaidia wajifunzaji kuimarika na kumudu matumizi ya Kiswahili katika muktadha halisi wa mawasiliano.

## MAREJELEO


- Akmal, S., Masna, Y., Tria, M., na Maulida, T. A. (2020). “EFL Teachers' Perceptions: Challenges and Coping Strategies of Integrated Skills Approach (ISA) Implementation at Senior High Schools in Aceh”. *Indonesian Journal of English Language Teaching and Applied Linguistics*, Juz. 4(2): 363-380.
- Alderson, J. C. (2000). *Assessing Reading*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Ali, K. A. (2021). *Tathmini ya Msingi wa Uhalisia katika Mitihani ya Kiswahili kama Lugha ya Kigeni: Mfano Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Zanzibar.
- Asafo-Adjei, R. (2022). “Testing the Four Basic Language Skills in the English LanguageComponent of the Mature Students' Entrance Examinations: The Case of SixGhanaian Universities”. *Mediterranean Journal of Social Sciences*, Juz. 13(1): 105-117. Inapatikana katika https://doi.org/10.36941/mjss-2022-0010.
- Bachman, L. F. (1990). *Fundamental Considerations in Language Testing*. Oxford: Oxford University Press.
- Brown, H. D. (2004). *Language Assessment: Principles and Classroom Practices.* New York: Pearson Education Inc.
- Davies, A. (1990). *Principles of Language Testing*. Massachusetts: Basil Blackwell Ltd.
- De Silva, R. (2020). “Assessment Literacy and Assessment Practices of Teachers of English in South-Asian Context: Issues and Possible Washback”. Katika B. Lanteigne C. Coombe na J. D. Brown (Wah). *Challenges in Language Testing Around the World.* Singapore: Springer Nature Singapore Pte Ltd. Kur. 433-446.
- Dörnyei, Z. (2001). *Motivational Strategies in the Language Classroom*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Douglas, D. (2000). *Assessing Languages for Specific Purposes*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Douglas, D. (2010). *Understanding Language Testing*. London: Hodder Education.
- Ellis, R. (1994). *The Study of Second Language Acquisition*. Oxford: Oxford University Press.
- Gardner, R. C. (1985). *Social Psychology and Second Language Learning: The Role of Attitudes and Motivation*. London: Edward Arnold.
- Gautam, P. (2019). “Integrated and Segregated Teaching of Language skills: An Exploration”. *Journal of NELTA Gandaki*, Juz. 1: 100-107.
- Goodman, N. D., Ullman, T. D. na Tenenbaum, J. B. (2011). “Learning a Theory of Causalitiy”. *Psychological Review.* 118(1): 110-119. Inapatikana katika https://doi.org/10.1037/a0021336.
- Hamad, F. H. (2020). *Tathmini ya Uthabiti wa Mitihani ya Kiswahili kwa Wageni: Mfano Mitihani kutoka Chuo kikuu cha Taifa cha Zanzibar*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Zanzibar.
- Hume, D. (1748) *An Enquiry Concerning Human Understanding*. London: A Millar.
- Kahindi, S. S. (2022). *Uwiano kati ya Malengo Mahsusi na Mazoezi ya Stadi ya Kuzungumza katika Darasa la Kiswahili kama Lugha ya Kigeni: Kitabu cha Zungumza Kiswahili Hatua ya Kwanza.* Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Zanzibar.
- Khosiyono, B. H. C. (2021). “Discrete and Integrated Approach and the implications on Language Teaching Learning management”. *Journal of English Studies*, Juz. 4(1): 19-29 Inapatikana katika https://jurnal.umk.ac.id/index.php/Pro
- Lantolf, J. P. na Poehner, M. E. (2004). “Dynamic Assessment: Bringing the Past into the Future”. *Journal of Applied Linguistics*, Juz. 1(1): 49-74.
- Lynch, B. K. (1996). *Language Program Evaluation: Theory and Practice*. Cambridge: Cambridge University Press.

- Mao, A. M. (2022). "Literature Review of Language Testing Theories and Approaches". *Open Access Library Journal*, Juz. 9: 1-5. Inapatikana katika https://doi.org/10.4236/oalib.1108741.
- Mgasho, M. S. (2020). *Mkabala unaotumika katika Utungaji wa Mitihani ya kiswahili kama Lugha ya Kigeni.* Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Zanzibar.
- Noroozi, M. na Taheri, S. (2022). "Task-based Language Assessment: A compatible Approach to assess the Efficacy of Task-based Language Teaching vs. Present, Practice, Produce". *Cogent Education,* Juz. 9: 1-21. Inapatikana katika https://doi.org/10.1080/2331186X.2022.2105775
- Oller, J. W. (1979). *Language Tests at School: A Pragmatic Approach*. London: Longman.
- Pearl, J. (2000) *Causality: Models, Reasoning and Inference.* Cambridge: Cambridge University Press.
- Power, D. E na Powers, A. (2014). "The Incremental Contribution of TOEIC Listening, Reading, Speaking and Writing test to predicting performance on real-life Language Tasks". *Language Testing*, Juz. 32 (2): 151-167. Inapatikana katika https://doi.org/10.1177/0265532214551855
- Richards, J. C. na Rodgers, T. S. (2001) *Approaches and Methods in Language Teaching* (Toleo la 2). Cambridge: Cambridge University Press.
- Rubanza, Y. I. (2010). "Masuala ya Msingi katika Utayarishaji wa Majaribio kwa Wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama Lugha ya Pili". *Kioo cha Lugha*, Juz. 8: 43-56.
- Semiun, T. T. na Luruk, F. D. (2020). "The Quality of an English SummativeTest of Public Junior High School, Kupang-NNT". *English Language Teaching Educational Jounal*, Juz. 3(2): 133-141. Inapatikana katika https://doi.org/10.12928/eltej.v3i2.2311
- Sevy-Biloon, J. (2018). "Integrating EFL Skills for Authentically Teaching Specific Grammar and Vocabulary". *Studies in English language and Education,* Juz. 5(2): 175-184. Inapatikana katika https://doi.org/10.24815/siele.v5i2.9705
- Shohamy, E. (2001). *The Power of Tests: A Critical Perspective on the Uses of Language Tests*. Harlow: Longman.
- Woodward, J. (2021) *Causation with a Human Face: Normative Theory and Dascriptive Psychology*. Oxford: Oxford University Press.


**Cite This Article:** Zitaamanzia Said Kididi & Michael Amri Mashauri (2025). Changamoto za Upimaji Jumuishi katika Ufundishaji wa Kiswahili kama Lugha ya Kigeni. *East African Scholars J Edu Humanit Lit, 8*(6), 250-259.